Jina……. **Nambari yako……/…….**

Shule…… **Sahihi yako……..……**

Tarehe ……..…

102/3
KISWAHILI
Karatasi ya 3
(FASIHI)
JULAI / AGOSTI - 2010
MUDA: SAA 2 ½

TATHMINI YA PAMOJA YA WILAYA YA MANGA - 2010

Kenya Certificate of Secondary Education (K.C.S.E)

102/3
KISWAHILI
Karatasi ya 3
(LUGHA)
JULAI / AGOSTI - 2010
MUDA: SAA 2 ½

MAAGIZO

1. Jibu maswali manne pekee
2. Swali la kwanza ni la lazima
3. Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja
4. Jibu maswali matatu yaliyobaki kutoka sehemu zilizobaki yaani Tamthilia, Riwaya, Hadithi fupi na Ushairi.

Karatasi hii ina kurasa 4 zilizopigwa chapa
Watahiniwa wanastahili kuona kuwa maswali yote yako na hakuna yaliyoachwa.

© 2010 Halmashuri ya Wilaya ya Manga

SEHEMU A: USHAIRI

1. Soma shairi A na B kisha ujibu maswali yanayofuata.

SHAIRI LA A

Nikiwa na njaa na matambara mwilini,
mmehudumika kama hayawani,
Kupigwa na kutukanwa,
Kimya kama kupita kwa shetani.
Nafasi ya kupumzika hakuna,
ya kulala hakuna,
ya kuwaza hakuna,
Basi kwani hili kufanyika.
Ni kosa gani lililotendeka,
Lilonileta adhabu hii isomalizika?
Ewe mwewe urukae juu mbinguni,
Wajua lililomo mwangu moyoni
Niambie pale mipunga inapopepea
ikitema miale ya jua
Mamangu bado anga1i amesimama akinisubiri?
Je nadhari yake hujitokeza usoni
Ikielekea huku kizuizini?
Mpenzi mama, nitarudi nyumbani
Nitarudi hata kama ni kifoni
Hata kama mauti yangu imekatikatika.
Vipande elfu, elfu kumi,
Nitarudi nyumbani,
Nikipenya kwenye ukuta huu,
Nikipitia mwingine kama shetani,
Nitarudi mpenzi mama……..
Hata kama ni kifoni.

SHAIRI LA B

<u>Baada ya dhiki faraja</u>

Yangawaje malelengu, mashaka yakutilie
Yatutia na tewengu, kuzipa nyoyo uwele,
Subira ni kilimwengu, mtu kuiweka mbele,
Hakuna tabu milele, baada dhiki faraji,

Lolote likikufika, yapasa uzingatile,
Ni amri ya Rabuka, mtenda hili na lile,
Mambo yanavyogeuka, na watu ni vile vile,
Hakuna tabu milele, baada dhiki faraji,

Leo huna kutukuka, kwa utajo wa riale
Vibindo vimefutuka, mifuko nayo tele,
Mpanda ngazi hushuka, kula bado na mawele,
Hakuna tabu milele, baada dhiki faraji,

Hali iwapo ni hii, mambo yakuzungukile,
Usiondoe bidii, fanya hima wende mbele,
Kwa mawazo usidhii, kudhani hivi na vile,
Hakuna tabu milele, baada dhiki faraji,

Fanya kwa kudhamiria, tabu ikuepukile,
Utazame kila nia, njema sio upotele,
Penye nia pana njia, ya kufikia vilele,
Hakuna tabu milele, baada dhiki faraji,

Mwenye kujisaidia, hutumika jambole,
Mungu humkusudia, msaada kwa tendole,
Mwisho akanipatia, sitawa huku na kule,
Hakuna tabu milele, baada dhiki faraji,

Basi vikikupotea, ulovitaka vikele,
Usikae na kulia, kutafakuri vya kale,
Karibu na baidia, vitafute pole pole,
Hakuna tabu milele, baada dhiki faraji,

a) i) Shairi la A huitwaje? (alama 1)
ii) Lipe kichwa kinachofaa(shairi A) (alama 1)
b) Mashairi haya mawili yana maudhui gani? Eleza ukitumia maudhui mawili mawili kutoka kila shairi. (alama 4)
c) i) Taja na utoe mifano minne ya tamathali za usemi zilizotumiwa katika mashairi yote mawili.
ii) Huku ukitoa mifano, eleza jinsi uhuru wa kishairi ulivyotumiwa katika shairi B (alama 2)
d) Fafanua arudhi za utunzi zilizotumiwa katika kulisarifu shairi la B.
e) Andika ubeti wa 3 wa shairi B kwa lugha ya nathari. (alama 4)
f) Eleza maana ya maneno haya kulingana na matumizi shairini
i) Kutafakuri
ii) Tewengu (alama 2)

SEHEMU B

TAMTHILIA – KIFO KISIMANI (Kithaka wa Mberia)
Jibu swali la 2 au la 3

2. ‘Asante. Jambo la pili ambalo limenileta ni kukutuma tena kwa Mtemi’

a) Eleza muktadha wa usemi huu. (alama 4)

b) Msemewa anatumia chuku na kinaya anapojibu. Eleza. (alama 4)
c) Mbali na kisa hiki, bainisha jinsi usaliti na ujinga ulivyodidimiza juhudi za ukombizi katika Butangi. (alama 12)

au

3. ‘Uchochezi wao utakuwa mbio za sakafuni.
Wanamchezea mamba’ Wanagusagusa mkia wa mamba! Ama kweli wao ni zaidi ya mazuzu. Ni punguani haswa!

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)

b) Msemaji anadhihirisha hulka zipi katika dondoo hili. (alama 3)

c) Eleza sifa nyinginezo za msemaji mbali na za dondoo hili. (alama 7)

d) 'Bila mchango wa wanawake ukombozi wa nchi ya Butangi ungalibaki ndoto'
Eleza huku ukitumia wahusika watatu. (alama 6)

SEHEMU C
RIWAYA – UTENGANO (S.A. Mohammed)
Jibu swali la 4 au 5

4. 'Mwiba wa kujichoma hauambiwi pole'
Thibitisha ukweli wa kauli hii huku ukirejelea riwaya ya UTENGANO. (alama 20)

Au

5. 'Ndoto na Sadfa ni mbinu za sanaa zilizofaulisha utunzi wa riwaya ya Utengano'
Eleza huku ukitoa maana ya ndoto hizo. (alama 20)

SEHEMU D
MAYAI WAZIRI WA MARADHI NA HADITHI NYINGINE.

6. a) Neno kumi limetajwa kwa maana mbali mbali katika hadithi ya Mayai Waziri wa Maradhi. Zitaje (alama 8)
b) Fafanua maudhui matano yaliyomshughulisha msanii wa Hadithi ya Mayai Waziri wa Maradhi. (alama 12)

SEHEMU E
FASIHI SIMULIZI

7. Jibu maswali kama ulivyoagizwa.
a) Taja vipera viwili vya mazungumzo katika Fasihi Simulizi. (alama 2)

b) Tofautisha dhana hizi
i) Visasili
ii) Miviga
iii) Mighani
iv) Misimu (alama 4)
c) Eleza umuhimu wa ngomezi . (alama 3)
d)i) Taja sifa mbili za vitendawili. (alama 2)
ii) Taja na ueleze majukumu mawili ya vitendawili. (alama 2)

iii) Taja sifa bainifu za ngano. (alama 2)
e) Eleza dhima ya nyimbo katika jamii. (alama 5)